

**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI**  
**KISWAHILI**  
**KIDATO 3**

**INSHA Alama 20**

1. Anza kwa: Mwanangu, dunia imebadilika pakubwa. Lakini chunga mabaduliko hayo yasikuzuzue.....

**MATUMIZI YA LUGHA**

1. Tofautisha sifa za vipasuo /p/ na /b/ (Al 2)
  - **/p/ ni sauti sighuna**
  - **/b/ ni sauti ghuna**
2. Ni sifa zipi zinazotumiwa kuchunguza jinsi konsonanti zinavyotamkwa? (al 3)
  - **Mahali hewa inapozuiliwa**
  - **Jinsi hewa inavyozuiliwa**
  - **Haki ya mtetemeko kwenya nyuzi za kutamkia sauti**
3. Tambua vielezi katika sentensi ifuatayo (al 2)
  - Hamali na kibe wataenda Mombasa kesho kutwa.
    - **Mombasa – Kielezi cha mahali**
    - **Kesho kutwa – kielezi cha wakati**
4. Tunga sentensi mbili mbili kuonyesha maana tofauti za maneno uliyopewa. (al 4)  
Mbazi – **Chombo / kifaa cha chuma chenye meno kinachotumiwa kukunia nazi**
  - **Mnyama anayefugwa**

**Mlango – Ukoo, nasaba au uzawa**

- **Sehemu inayogawanya kitabu, sura**
- **Kizuizi cha kuziba uwazi wa kuingilia na kutokea kwenye nyumba**

Kadiria jibu la mwanafunzi

5. Akifisha sentensi ifuatayo (al 3)
  - Bwana baraka huenda mjini kila jumapili kutazama mchezo wa kuigiza wa vioja mahakamani.
    - **Bwana Baraka huenda mjini kila jumapili kutazama mchezo wa kuigiza wa “vioja mahakamani.”**
6. Bainisha aina za maneno katika sentensi zifuatazo (al 4)
  - (i) Cheti cha pamoja kimepatikana  
N            V            T
  - (ii) Lo! Fisi amepanda juu ya mti  
T    N      T        H    N

7. Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo (al 2)  
Zubeda alimwandikisha Ali barua
  - **Zubeda alimlazimisha Ali aandike barua**
  - **Zubeda alimsaidia Ali kuandika barua**
8. Tambua nyakati katika sentensi zifuatazo (al 2)
  - (i) Jana kulinyesha mvua kubwa  
**Li – wakati uliopita**
  - (ii) Mimi ninajibu maswali  
**Na – wakati uliopo**
9. Tumia kirejeshi ‘amba ‘badala ya ‘o’ rejeshi katika sentensi ifuatayo. (al 2)  
Uwanja ulipandwa miti ni wa mjombangu
  - **Uwanja ambao ulipandwa miti**
10. Akifisha sentensi ifuatayo ili iwe katika hali tatu tofauti. (al 3)
 

Rais amewasili

  - (i) **Rais amewasili. (taarifa)**
  - (ii) **Rais amewasili? (swali)**
  - (iii) **Rais amewasili! (mshangao)**
11. Eleza ritifaa imetumika vipi katika sentensi (al 2)
  - (i) Ngombe wa jirani amepotea
  - (ii) Nilimwonya `ngawa hakun`sikia
  - **Kuonyesha sauti zenyenye ving'ong'o**
  - **Kuonyesha maneno yamefupishwa: `ngwa**
12. Kanusha sentensi ifuatayo; (al 2)
 

Sungura amekufa

  - **Sungura hajafa**
13. Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika kauli ya kutendea (al 2)
  - (i) Kasiva aliandika barua ya indeche
    - **Kasiva alimwandikie indeche barua**
  - (ii) Msetu alikula chakula cha mtoto
    - **Msetu alimlia mtoto chakula**
14. Andika sentensi zifuatazo kwa udog (al 2)
  - (i) Mji huu una watu wengi
    - **Kijiji hiki kina vijitu wengi**
  - (ii) Meza yangu kubwa imevunjika
    - **Meza yangu kubwa kimevunjika**

#### **SEHEMU C: ISIMU JAMII**

Long'i ni mia, pata na mia, pata na mia, hundred bob tu, kuona ni bure. Viatu ni za aina yote. Buda karibu ujionee. Niaje maze come tu..... Come tu, karibia ujionee. Hata za manzi ziko. Mali motomoto kutoka ng'ambo. Watu wote wabuy huku! Dungarees ni soo mbili.....za watoi na wasupa.

- (a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya. (al 2)
- **Ni lugha ya sokoni, muuzaji akiwaita wateja kwa kunadi vitu vyake**
- (b) Eleza sifa za lugha itumiwayo katika sajili hii kama zinavyojitokeza katika kifungu.
- (i) **Lugha yenye makosa mengi ya kisarufi. Km: viatu ni za aina yote.**
  - (ii) **Lugha shawishi ili kuwavutia na kuwashawishi wateja mf. Kuona ni bure, mali motomoto kutoka ng'ambo na watu wote wanabuy huku.**
  - (iii) **Ni rahisi kueleweka kwa sababu ya muundo wake wa sentensi fupifupi.**
  - (iv) **Ina chuku ili kuvutia wateja mf. Mali motomoto kutoka ng'ambo na watu wote wanabuy huku.**
  - (v) **Ina porojo nyingi kwa mfano muuzaji anapoimba wimbo wa pata na mia.**
  - (vi) **Ina kukariri kwingi kwa mfano muuzaji anarudiarudia pata na mia na come tu.**
  - (vii) **Kuna kuchanganya ndimi kwa mfano, matumizi ya maneno 'hundred' na 'come'.**
  - (viii) **Lugha ya mitaani hutumiwa, k.m maneno 'mzae' na 'manzi'.**